# UQAB

Jarida la




*Toleo 38- Rajab 1441 H / MACHI 2020 M*



1. **BBI– WALA SI MCHEZO WA MWISHO WAKUMALIZA UFISADI Uk.2**
2. **JE BBI ITAWEZA KUWAFUNGAMANISHA WATU WA TAIFA LA KENYA Uk.5**
3. **BBI NA SIASA ZA MWAKA WA 2022 Uk.9**




## HIZB UT TAHRIR KENYA BBI KAMPENI

## # BBI MCHEZO NI ULE ULE MBINU MPYA

uqab.or.ke uqab_htk UQAB-Magazine-1911964012162253

BARUA PEPE: info@uqab.or.ke JARIDA LA UQAB1

# BBI-WALA SI MCHEZO WA MWISHO WA KUMALIZA UFISADI




**Habari**

Mnamo tarehe 27th Novemba, 2019 jopo kazi la BBI pamoja na viongozi wa kisiasa waliitangazia wazi kwa umma repoti ya BBI. Ndani mwa repoti hio ilibainika kuwa ufisadi ni miongoni mwa mambo tisa yaliokuwa na umuhimu kuangaziwa iwapo taifa lingependa kustawi. Katika mlango wa nane wa repoti hio, ufisadi uilijadiliwa na mapendekezo juu yake kutolewa ikitarajiwa kwamba laiti yatatabikishwa basi ufisadi utakuwa ni jambo la kusahauliwa.

**Maoni:**

Kutoka kubuniwa kwa taasisi ya ufisadi hadi kubuniwa kwa nambari za mawasiliano za dharura, kwa kweli mengi yamependekeza na kutekelezwa lakini hayakuweza kuangamiza ufisadi.

Mnamo Jumatatu tarehe 11 Aprili, 2016 katika juhudi za kupambana na ufisadi, Macharia Gaitho alipendekeza katika makala yake kwenye gazeti la Nation ya kwamba **“Pengine twahitaji kuomba suluhu la Uchina dhidi ya ufisadi.**” Hata hivyo suluhu hili la Uchina limebainika ya kwamba si la uhakika. Kwa mujibu wa gazeti la Daily Telegraph ni kwamba mapambano juu ya ufisadi Uchina licha ya kuwa na sharia kali dhidi yake hayajapelekea kupungua visa vya ufisadi. Wachambuzi wasema ya kwamba kampeni hio ilikuwa haina uwazi na ilikuwa tuu njia moja wapo ya kuwaondoa mahasimu katika nafasi nyeti.

Katika miaka ya nyuma, serikali iliamua kutekeleza mapendekezo ya kuimarisha taasisi zake kama njia mmoja wapo ya kupambana na ufisadi.Kwa hivyo, sharia mpya zikatawazwa na taasisi kuwezeshwa na rasilimali pamoja na kuwa huru na mamlaka yakutosha. Mnamo katika masiku ya kongamano la mapambano dhidi ya ufisadi yaliokuwa yameandaliwa ikulu ya Nairobi mnamo tarehe 18 Octoba, 2016, viongozi tofautu wa taasisi za umma walihojiwa juu ya vipi mapambano ya ufisadi hayaja leta natija licha ya yote? Walijibu kwa kutupiana lawama juu ya taasisi ipi ndio ilikuwa kisiki

juu ya kufaulu kwa mapambano ya ufisadi. Kupitia mchezo wa kulaumiana, taasisi mbali mbali ziliashiria kwa namna gani haziwezi kupambana na ufisadi licha ya kuwezeshwa kwa hali ya juu. Katika onyesho la fedhea kwa kushindwa vita dhidi ya ufisadi licha ya kujihami na katiba mpya, raisi aliinuka na kusema**,"Nimechukuwa hatua ambazo zilitulazimu kwa mujibu wa katiba,hivyo mnataka nifanye nini tena?"** Kwa kweli matokeo ya kongamano hilo la mapambano dhidi ya ufisadi yaliashiria kwamba kuwepo kwa taasisi za umma zilizo kuwa huru na kutoshelezwa kirasli mali si tuu ni suluhu dhidi ya vita vya ufisadi.

Katika muhula wake wa pili wa utawala raisi Uhuru huku akiwa na matumaini ya kufaulu, aliamua kupambana upya na ufisadi kwa kubadilisha viongozi mbali mbali wa taasisi zinazo husika na mapambano dhidi ya ufisadi.



Kwa kuashiria kupendezwa na mbinu hii, raisi alisema**," Baada ya kusafisha afisi ya DPP na DCI,sasa tuna timu inayo ajibika.Mumeanza kuona maovu makubwa yakifichuliwa nah ii ni mwanzo tu, Bado hamujaona chochote."** Lakini kwa mbinu hii kupatikana mapendeleo ndani yake, baadhi ya viongozi wa kisiasa pamoja na jamii zao walisusia juhudi hii mpya dhidi ya ufisadi. Naibu wa raisi Ruto mwenyewe alisikika akikosoa namna kiongozi wa kuendesha mashtaka wa umma Bw. Haji na yule wa uchunguzi wa uhalifu Bw.George Kinoti walivyokuwa wakifanya kazi zao kwa kuwa na mapendeleo ya kulenga watu fulani pekee. Katika hotuba yake kwenye kongamano la LSK Huko Mombasa, Naibu wa raisi alisema**," Vita dhidi ya ufisadi ambavyo vimekosa uadilifu hupotea kuwa ni vita dhidi ya ufisadi bali enyewe huwa ufisaidi kamwe.Vita ambavyo havina uadilifu huwa ni kutokujali.Vita adilifu vinavyopiganwa kwa kuchaguwa, kutumia ukweli nusu, na kuwepo maono tayari ya kisiasa kwenye bongo, ni vita vya kutokujali."**

Kwa ufupi, mapambano dhidi ya ufisadi hayatoweza kushindika kwa kupitia njia zilizobuniwa na mfumo wa kirasilimali kwa kuwa ni urasilimali ndio asili umewafanya watu kuwa wafisadi. Pindi Urasilimali ulipotengamanisha mada na roho, na kufanya uchumaji wa vitu vya kushikika ndio lengo kuu la maisha, na kipimo cha vitendo ni maslahi, basi ilikuwa ni jambo la kimaumbile ya kwamba ufisadi utakuwa ndio mtindo

wa maisha wa jamii. Laiti mada haingetenganishwa na roho, basi mtu angelikuwa saa zote ni mwenye kutanabahi fikra ya kutunzwa na kuadhibiwa, kupata pepo au moto, kuwa na vitendo vyema au viovu kabla ya kutekeleza vitendo. Laiti akili haingelifanywa ndio chimbuko la kutunga sharia, mwanadamu angeli hukumu katika maisha yake kwa mujibu wa kile allicho amrisha Maulana na kwa hivyo ufisadi ugelikuwa ni jambo la kale kwani sharia za Maulana zingeleta uadilifu na amani. Licha ya hivyo, laiti mwanadamu angelifanya msingi wa matendo yake ni kupata radhi za Mola wake na wala si vitu vya kushikika basi mwanadamu angelikuwa amelindwa kwa kutekeleza mazuri na kuepuka maovu yakiwemo ufisadi.




Katika jinamizi hili la kutoelewa ni kwa jinsi gani nzuri twaweza kuangamiza ufisadi hususan baada ya kumaliza kutekeleza mapendekezo kwa mapendekezo, imefika wakati muafaka kwa watawala kusikiza sauti za ndanii zilizo kamilika za kisiasa za kiisilamu. Kama vile ilikuwa wajibu kwa wao kutabani na kutabikisha sehemu chache ya fikra ya nidhamu ya fedha ya kiisilamu, basi nyakati imefika iwe si tuu kuchukuwa sehemu katika islamu bali imefika wakati kuchukuwa uwongozi kamili wa kififikra ya kiisilamu kwani kwa uhakika ni uisilamu pekee ndio badili ya mfumo wa kirasilimali ambao ndio chanzo cha ufisaadi.

**“Na inaposemwa kwao wao,”Musifanye uharibifu katika ardhi, ’’wao husema, “Siwe ni watengenezaji.”** TYQ 2:11

ABU LEILA 2020

# JE BBI ITAWEZA KUWAFUNGAMANISHA WATU WATAIFA LA KENYA ?

BBI Building Bridges Initiative

## KUTOKA TAIFA LA MAHUSIANO YA DAMU HADI MAHUSIANO YA MAADILI

Mnamo Jumanne 27th Novemba 2019, wakenya kutoka sehemu mbali mbali walijumuika Bomas ya Kenya na kusherehekea kwa kutangaziwa rasmi repoti ya BBI kwa wananchi. Repoti hio ya kurasa 156 ilikuwepo na agenda tisa na kauli mbiu yake ikiwa: **Kujenga Daraja hadi kuwa na Kenya ilio moja: kutoka taifa lililo fungamanishwa na damu hadi kuwa taifa la maadili.** Katika kurasa zake za mwanzo za repoti hio, Jopo kazi la BBI lilimuandikia raisi kwa kusema**," ilikuwa fursa dhahabu kwetu , na kwa uweza tuliopewa wa kubaini husuba za taifa kamavile ilivyo tambulishwa katika kauli ya pamoja ya Ujezi wa Daraja kwa taifa jipya la Kenya, na baada ya kutekeleza wajibu huo, basi tume pendekeza mapendekezo ambayo yatajenga umoja wa kudumu."** Katika mazungumzo yake mnamo siku ya kutangazwa rasmi repoti ya BBI, raisi alisema**," Hebu tu shughulike na lile linalotuunganisha sisi na kuwa wa moja na hebu tuondoe ukabila,"**

Kwa kutizama hayo yalio juu, inabainika ya kwamba mchakato wa BBI unafikiriwa kuwa ni wenye kuita watu kuwa kitu kimoja. Kwa hakika mwita wa, umoja na utafutaji wa juhudi za kuwaungamanisha wakenya si jambo geni. Mnamo jumapili tarehe 6 Septemba 2016 kiongozi wa wabunge wengi, Aden Duale katika mkutano hapo Mlango Kubwa alisikika akisema**," Kura za mwaka wa 2017 zitakuwa ni kati ya Jubilee ambayo inaamini umoja wa makabila 42 na wale ambao wapo tu huko kugawanya watu kwa siasa za kikabila."** Kwa kutumia jukwaa hilo hilo,Bwana sakaja nae kasema**," Ni wakati sa hii yatulazimu tuseme hapana kwa ukabila kwa jina la chama cha kisiasa. Jubilee imekuja kuwaunganisha wakenya**

**chini ya kivuli kimoja."** Katika masiku ya kuzindua rasmi chama cha Jubilee hapo kasarani, Kiongozi wa chama Bwana Kenyatta alisema**," Chama tunacho kizudua hapa leo ni kuashiria umoja wetu."**

Hivyo basi yaashiria ya kwamba kuwa hapo nyuma, viongozi wa kisiasa waliamini kuwa umoja ungelipatikana tu kwa kupitia vyama vya kisiasa.

Sawia na hayo, miito hio ya umoja iliwahi kusikika mwakani 2008 wakati taifa lililikuwa limetoka katika majeraha ya vita baada ya uchaguzi mkuu. Kwa kupitia mdahalo wa maridhiano na matangamano wa Kenya, raisi Kibaki na Raila Odinga walitia saini makubaliano ya utabikishaji wa mapendekezo ya jopo kazi la uchunguzi wa vita vya baada ya uchaguzi wakitarajia kuwa kufanya hivyo ndio wataleta amani ya kudumu milele.

Umar ibn al Khatatab {r.a}, Khalifah wapili wa waisilamu alisema,**'' Hapana uisilamu bila umoja, na hapana umoja bila uwongozi na hapana uwongozi ila kuthwii,"** Kutokana na kauli hii yaeleweka kwamba kuwepo kwa taifa lelote lile hutegemea umoja wa watu kwa taifa hilo. Zaidi ya hivyo, ili taifa liweza kupata matunda ya mafanikio, halina budi liwe na umoja baina ya umma wake. Kwa hivyo ni jambo lisilo staajabisha kuona ya kwamba mataifa yote yata ngangana kuhakikisha umoja kati ya umma zao umepatikana ndani yao.

Tangu nchi za Afrika zipate uhuru, zimekuwa zikitambua ya kwamba umoja kati ya makabila yao wapatikana ima kwa kupitia vyama vya kisiasa au midahalo ya amani. Kwa kweli mtazamo huu umepelekea kuona baadhi ya nchi zingine zikibuni chama kimoja cha kisiasa, au kuunganisha vyama vyingi vya kisiasa na au kubuni midahalo ya umoja na amani ambayo huishia kwa kusainia mikataba ya amani na pia kuleta marekebisho ya katiba. Kutokana na msingi huu muovu wa kuleta watu pamoja, imekuwa ni jambo la kimaumbile kuona mara kwa mara nchi kuwa na mfazaiko na kutishiwa kuangamia. Mito ya kujitenga, vita baada ya kura za uchaguzi, chuki za kikabila, zote hizi ni mifano moja wapo inayoonyesha jinsi gani watu wa Afrika hawana umoja. Kwa kweli ni kwa ihsani ya wakoloni wa magharibi ndio twapata kuona nchi za Afrika zina umoja ndani mwao.

Ni jambo la hakika ya kwamba vyama vya kisiasa si vyombo vya kufungamanisha watu katika nchi. Lazima itabulike kuwa kazi ya vyama vya kisiasa ni ku kampeni na kusajili

wagombezi ili waweze kushikilia afisi za usimamizi na pia wawe ni wenye kuhisabu serikali kuu.

Vile vile, michakato na midahalo kama vile BBI haijakuwa ni vyombo halisi vya kuleta utangamano wa kudumu. Hi ni kwasababu msingi iliyo simamo kwayo huwa ni maslahi ya mtu binafsi hivyo basi pindi maslahi hayo ni yenye kukosekana nao umoja pia ni wenye kukosekana. Kwa kuwa BBI ilibuniwa kwa ihsani ya viongozi wawili, basi litakuwa ni jambo la kimaumbile kuona ya kwamba BBI itapingwa vikali na kugawanya watu zaidi maadamu maslahi ya watu wengine mbali na ya wawili hao waasis hayakutiliwa maanani. Na hili lilikuwa wazi pindi siku ilipokuwa yazinduliwa rasmi repoti ya BBI. Bwana Senator Murkomen alisikika akisema siku hio**, " Kwa njia Bwana Mohamed anavyoendesha shughuli hii ina shinda malengo halisi ya mjumuiko huu. Ni wazi kuwa wale ambao waoyesha wana maono tofauti hawaja alikwa kuja kuzungumza."**



Hili basi la tibitisha ya kwamba BBI itagawanya watu zaidi badala ya kuwaugamanisha. Alipokuwa ni mwenye kuzuru huduma ya kanisa hapo Full Gospel Gatunduri Church Embu, William Ruto alisema kuwa BBI itasimamishwa iwapo itaendelea kuwagawa waKenya**." Hii stori twasikia eti hakuna mtu anaweza simamisha rege, ikiwa rege ni ile tunaona ukabila unao pigiwa debe katika mikutano ya BBI, Kukagua makabila, chuki na kugonganisha jamii moja kwa nyengine, ikiwa hio ndio rege wanaiongelea, rafiki zangu, rege itasima,"**

Kwa kutamatisha, mchakato wa BBI kamwe hautaweza kuleta umoja wa kudumu ila uhasama. Jambo ambalo hakika litawezesha umoja upatikane ni kuwepo kwa mfumo ambao ndani yake kunapatikana nidhamu. Pindi watu watakapo amini nakutabikisha mfumo inatarajiwa kwao wao kuwa na fikra, hisia na nidhamu mmoja. Ule uwepo wa watu kuwa na hisia, fikra na nidhamu mmoja hujaalia watu wakawa ni wa moja nyakati zozote maishani

Ili ndoto hii iweze kupatikana, ndoto ya kuwezesha taifa liwe taifa la kimfumo haina budi kufanyiwa jazi. Kwa minajili ya kuwepo kwa umoja katika taifa, viongozi wa kisiasa lazima wazidishe kutilia nguvu miito ya kubandua nchi zao kuwa nchi za kiutumwa zinazo zunguka madola makuu ya kimfumo. Sauti za kikweli hizi ndio hatimae zitapelekea taifa kuwa la kimfumo na wananchi kuwa na umoja daima.

**ABU LEILA 2020**

# BBI NA SIASA ZA MWAKA WA 2022



Kujiapisha Raila Odinga kama rais wa watu March, 2018 ilikuwa ni hatua ya kutuma ujumbe kwa utawala wa rais Kenyatta wa kuwepo na nafasi ya mazungumzo. Natija yake ni kupatikana kwa Handshake iliyozaa jopo kazi la mradi wa ujenzi wa madaraja BBI uliochapishwa kwenye gazeti rasmi la serikali tarehe 24 Mei 2018. Siku ya Jumanne tarehe 26 Novemba, 2019, viongozi hao wawili wakapokea rasmi ripoti ya BBI. Siku ya Jumatano 27 Novemba, 2019 ripoti hiyo ikazinduliwa rasmi kwa umma.Hii ni baada ya jopo kazi kuchukua maoni ya baadhi ya wakenya kuhusu ajenda tisa ambazo zote kwa ujumla zinazungumzia kuboresha mfumo wa uongozi, mabadiliko ya kiuchumi upendeleo, ufisadi na utangamano.

Wengi wasiojua uhalisia wa siasa waliamini kwamba muundo wa tume ya BBI ni wa kuleta marekebisho au ni ripoti ya kiufundi technical report bali. Kiuekweli ukiangalia wanajopo wengi wa BBI utakuta wengi wao ni washauri wa kisiasa wa zamani na wasasa wa vigogo hawa wawili. Hii ni kumaanisha wawili hao ndio walielekeza BBI na kuiamulia mchakato wake. Kusajiliwa kwake katika gazeti rasmi kulimaanisha kwamba ni mradi wa serikali ambao itatumia rasilimali zake katika kuchakata michakato yote. Hivi ndivyo ilivyokuwa, shilingi takriban Bilioni 10 zilitumika katika kuandaa ripoti ya BBI. Ni dhahiri shahiri kwamba BBI ni mradi wa kisiasa unaohusiana na suala la kurithiwa kwa Uhuru Kenyatta. Hakuna shaka William Ruto na Raila Odinga wana nia ya kutaka kurithi Uhuru Kenyatta. Japo Raila Odinga hajasema yeye mwenyewe binafsi lakini kauli za wandani wake zinaashiria kuwa yeye huenda akangangania tena kwenye kinyang’anyiro cha urais. Kama vile Ruto anaimani kwamba yeye ataibuka kidedea katika kupeperusha bendera ya kuwania urais.

- ‘Handshake’ na BBI

Raila amekua kifua mbele katika kuuza BBI kwa raia na amekua akitumia mbinu inayojulikana kama **“Mfuato wa umaarufu”** Mbinu hii amekua akiitumia sana katika kampeni zake na kufaulu kuteka watu. Suala la BBI limekua ni mmoja wapo ya mkakati mpya wa Raila Odinga na hii ni kama alivyosema yeye mwenyewe kwenye mazishi ya mama wa aliekuwa mbunge wa GEM Joe Donde: **“Mumeniona mimi nikibadilisha mbinu, hu ni mkakati.Kuna njia nyingi za kutuongoza hadi kwa matamanio yetu pale yalipo.”** Kupitia kwa BBI anaonekana kupanga timu inayowahusisha watu kama vile Ann Waiguru, Wyclife Oparanya, Fred Matiang’I na Eugen Wamalwa.

Mbali na haya kuna kwa kuruhusu maazimio ya watu wa pwani kama yalivyosomwa na Amazon Kingi ni kuuitia sura zaidi ya kitaifa na wala isionekana ni mradi wa watu wawili. Hatua hii ya Raila imetia kiwewe wana Tangatanga wanaolalia upande wa naibu rais William Ruto walioana kwamba ajenda ya BBI itakwaza maslahi yao ikiwemo uwaniaji wa urais.

- Siasa za Mlima Kenya

Mwaka 2016, William Kabogo alipasua mbarika kwa kusema kwa Ruto atahitajika kufanya kazi ya ziada kutafuta kura za wakikuyu. Baada ya kaimu mwenyekiti wa Jubilee David Murathe kujiuzulu, aliwahutubia wanahabari Januari 2019 kwa kusema*:* **“sahii naona ya kwamba ni vigumu kuwa naibu wa mwenye kiti wa chama, hususan ikiwa nitakuwa naketi pkatika mkao wa Jopo ka Kitaifa la chama na mtu ambae nampeleka kotini kumzuia asigombee,"**Aidha, ashawai kusema kwamba eneo la Mt Kenya halina deni na Ruto.

- Vita dhidi ya Ufisadi.

Kuna lalama nyingi sana za wandani wa Ruto kwamba vita dhidi ya ufisadi vinalenga Ruto. Oscar Sudi na senata Murkomen wamekua wakimtaja mkurugenzi mkuu wa uchunguzi wa makosa ya jinai George Kinoti kuwa anatumiwa kumpiga vita Ruto. Akihutubia kongamano la LSK Mombasa, Ruto alisema:“ **Vita dhidi ya ufisadi ambavyo vimekosa uadilifu hupotea kuwa ni vita dhidi ya ufisadi bali enyewe huwa ufisaidi kamwe.Vita ambavyo havina uadilifu huwa ni kutokujali.Vita adilifu vinavyopiganwa kwa kuchaguwa, kutumia ukweli nusu, na kuwepo maono tayari ya kisiasa kwenye bongo, ni vita vya kutokujali**.” Yaliyofanywa Sonko na hivi punde Ferdinad Waititu yamechochea upande wa Ruto kuona ni jaribio la kukwaza kampeni za Ruto. La muhimu kufahamu ni kwamba rasilimali ni muhimu sana katika siasa na uchaguzi. Hivyo vita hivi ni kumdhoofisha Ruto uwezo wake wakifedha asiweze kuzitumia katika kununua watu na kujifanyia kampeni kisiasa mbinu hii huitwa sera ya kudhibiti

Kimantiki ukiangalia mapendekezo yote ya BBI utafahamu hakuna ajenda mpya ndani yake ila ni karata nyengine ya kisiasa inayochezwa na wababe wa kisiasa dhidi ya raia.

Ukitafakari kwa kina utatambua kuwa mapendekezo yote hayo kiasili ni majukumu ya serikali kuyatekeleza. Hii ina maanisha kazi ya serikali ni kusimamia raia wake waweze kufikia mustawa wa juu ya kiuchumi na kijamii masuala yasohitaji tume wala ripoti.



Kwenye hotuba yake katika mkutano uliofanywa Mama Ngina Water Front Jijini Mombasa Raila alisema**:"Hakuna awezae simamisha rege"** kumaanisha ngoma inayopigwa na vigogo wa kisiasa hakuna budi ila raia wataicheza tu! Mwandishi wa Makala Dkt Wandia Njoya amaitaja BBI kama Tangazo la vita la wababe wa kisiasa dhidi ya raia wababe wa kisiasa" **angazo la vita la wanasiasa dhidi ya raia**".

Kwa kuwa raia wengi wana ukosefu wa kile kiitwacho ufahamu halisi wa kisiasa **'utabuzi wa kisiasa'** basi wanasiasa hupatiliza hali hii na mara kwa mara huwahadaa wa kuwawekea raia mbeleni suluhisho walitakalo wao wanasiasa. Fauka ya haya matatizo yanayokumba jamii nzima leo licha ya kuwa yamesabishwa na mfumo muovu wa kibepari unaofaidi tu tabaka la kisiasa, raia kwa upande wao siku zote huwa na kiu cha mabadiliko na hapo ndipo wanasiasa hupatiliza kuwazushia ajenda zinazoteka hisia zao.

Tofauti za wanasiasa zinazoibuka kila wakati na hasa kwenye ajenda za kisiasa ni tofauti za kimaslahi baina yao wala sio kwa msingi wa kujali maslahi ya raia. William Clay alisema;**'Huu ni mchezo tuu. Katika siasa hakuna maadui wa kudumu wala marafiki wa kudumu bali yaliyoko ni maslahi ya kudumu".**

Mantiki ya maneno haya ni kwamba wanasiasa hutofautiana na kukubaliana kwa maslahi hivyo tofauti zao haziko katika kujali wala kulinda maslahi ya umma. Kambi moja ni ile inayotaka kudhibiti hali ilioko inayowafaa status-quo na upande mwingine ni kutaka kuibadili hali hiyo iweze kwenda watakavyo wao ili ioane na maslahi yao. Cha msingi kwenye kung'angania madaraka wao hutumia mbinu za kufarikisha raia kwa kuwapandikiza chuki za kieneo na kikabila hivyo hawa katu lengo la kuunganisha umma.

**Shabani Mwalimu**

**MWAKILISHI KWA VYOMBO VYA HABARI**

**HIZB UT-TAHRIR KENYA.**

**Afisi ya Habari**
**Hizb ut Tahrir**
**Kenya**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

**REF: 1441 / 07 H** Ijumaa 20th Jumadah II 1441 H **14/02/2020 M**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## UZINDUZI RASMI WA KAMPENI KUBWA YA HIZB UT-TAHRIR KENYA CHINI YA KAULI MBIU: BBI: MCHEZO ULEULE MBINU MPYA

Harakati ya Hizb ut-Tahrir Kenya inafuraha kuanzisha rasmi kampeni kubwa itakayodumu kwa muda wa miezi mitatu yenye kauli mbiu "BBI mchezo uleule Mbinu Mpya" inayoanza Jumamosi tarehe 15th Februari,2020 na kumalizika tarehe 24th Mei 2020.

Ripoti ya mradi wa ujenzi wa madaraja iliosajiliwa katika gazeti rasmi la serikali tarehe 24th Mei 2018 na kuwekwa wazi kwa umma kuisoma mwezi Novemba mwaka jana, inadaiwa kuwa ni mwanzo mpya unaodhaniwa kuleta sera za ushirikishi, mabadiliko ya kiuchumi na kutatua tatizo la siasa za kibwenyenye na ufisadi – matatizo ambayo yamekuwa ni yenye kuikabili Kenya zaidi ya nusu karne. BBI ambayo tayari imeibua tafrani miongoni mwa tabaka la kisiasa inakuja baada ya mwongo mmoja tu wa uzinduzi wa katiba ilioleta mfumo mpya wa utawala wa kiugatuzi na bado nchi inakumbana na matatizo hayohayo.

Kampeni hii inalenga kuangazia kiini na chanzo halisi cha majanga yote yanayoikabili Kenya na ulimwengu kwa ujumla ambacho si chengine ispokuwa ni Mfumo wa kikoloni wa kibepari na siasa yake ya Kidemokrasia inayotanguliza zaidi maslahi ya tabaka la wanasiasa na kupuuzilia mbali maslahi ya walala hoi wanaondelea kusugua maishani. Kampeni hii aidha inanuia kutoa taswira halisi ya nguvu ya itikadi ya Kiislamu katika kuunganisha jamii kwa mshikamano wa kudumu na kuwa wote ni umma moja na waja wa Mwenyezi Mungu (swt), pia kutatua matatizo ya kiuchumi,kisiasa na kijamii ambayo hayakabili tu jamii ya Kenya bali jamii zote duniani.

Katika kufanya kampeni hii, Hizb ut-Tahrir Kenya itaandaa misururu ya amali ikiwemo darsa kubwa katika maeneo mbalimbali, mazungumzo ya mitaani, semina za wasomi na mufakirina miongoni mwa amali nyengine.

Mwisho, tunatoa mwito kwa umma jumla na hasa umma wa Kiislamu kushiriki nasi katika kampeni hii tukufu ambayo tutajikita ndani kueleza mengi yenye kuleta manufaa sio ya hapa duniani bali pia Akhera.

Fuatilia Kampeni hii kwa Hashtag **:#BBI Mchezo Uleule Mbinu Mpya**

Shabani Mwalimu
**MWAKILISHI KWA VYOMBO VYA HABARI**
**HIZB UT TAHRIR IN KENYA**

[redacted]







BBI OLD GAME NEW STRATEGY
Colonialism
Independence
Peoples Constitution
Elections of 2007-2012
Multipartism
Prime Minister
Moi's removal
Election violence 2007
One Party
Now BBI
The Ndung'u report
Old constitution
TJRC
Election violence 97/98
Colonialists constitution
Wako / Wanjiku
ISLAM IS THE SOLUTION